


# HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: Na. 027-2660501  
Fax: Na. 027-2660500  
Barua pepe: Info@mkingadc.go.tz  
Tovuti: www.mkingadc.go.tz



S.L.P. 6005,  
TANGA.

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. HW/MKG/D.35/27/179**

**11.03.2022**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI 335 YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Kata, Vijiji na Vitongoji vya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

### **A. SIFA ZA WAOMBAJI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 mpaka 45
- ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- iii. Awe anamiliki simu janja Android (kuanzia 8.5 version) yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima. Aidha, simu janja hiyo Android isiwe aina ya Iphone.
- iv. Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi
- v. Awe ni mkazi wa Kata husika na awe tayari kutekeleza majukumu ya zoezi husika katika Kijiji chochote kilichopo katika Kata hiyo.
- vi. Awe na uwezo wa kutambua na kusoma ramani za eneo analoishi

### **B. KAZI NA MAJUKUMU**

- a. Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- b. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- c. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi

